BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 11 Juni, 2025

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

62. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Serikali inatoa tahadhari juu ya majanga yanayotokea katika maeneo ya nchi kavu na baharini na kuweka mkakati wa uokozi pindi yanapotokea.

    Ni njia zipi za dharura zinazotumika za kuwanusuru wananchi wetu katika maeneo mbali mbali.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

53. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Serikali ilikuja na mpango wa kuvikodisha baadhi ya visiwa kwa wawekezaji ili kuleta maendeleo kwa nchi yetu. Pamoja na mpango huo kuanza kutekelezwa, yapo malalamiko kuwa

vipo baadhi ya visiwa kama kisiwa cha Fundo ambavyo vinaishi watu na vimeingizwa katika mpango huo wa Serikali.

(a) Kwa tathmini ni visiwa vingapi ambavyo vipo kwenye mpango huu na vinaishi watu.

(b) Ni upi mpango wa Serikali kwa wananchi wanaoshi katika visiwa hivi kama kisiwa cha Fundo na vyenginevyo.

(c) Ni kiasi gani cha fedha kimepatikana katika ukodishwaji huu wa visiwa na kimetumika katika eneo gani.

<u>**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**</u>

171. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ni kwa namna gani Mhe. Rais anaweza kuwekewa vielelezo vya alama za kumbukumbu kwa mchango mkubwa anaoutoa katika sekta nzima ya mabadiliko ya kiuchumi.

255. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Miongoni mwa faida zinazopatikana kupitia ziara za kidiplomasia za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni kupata misaada ya kimaendeleo.

Ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kama msaada kwa Zanzibar kwa kipindi hiki cha miaka minne.

<u>**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**</u>

77. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kuna vitalu ambavyo Wizara yako huatika mbegu na baadae kuwafikishia wananchi ili wazipande katika mashamba yao.

(a) Je, upatikanaji wa mbegu uko vipi kwa sasa na Wizara yako inaatika mbegu za kutosha katika vituo vyake vyote.

(b) Ni nyenzo zipi mnazotumia kuzifikisha mbegu hizi katika vituo vya vitalu vyenu.

(c) Kuna mkakati gani wa Serikali kwa wananchi kupata mbegu zenye ubora.

93. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa vipi na kwa utaratibu upi elimu ya Kilimo Mkataba inaweza kumsaidia mkulima kujikwamua na umasikini.

<u>**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**</u>

14. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Gari la matangazo (PA) la ZBC Pemba limeharibika kwa siku nyingi sasa, hali inayopelekea kukosekana kwa huduma za matangazo kwa uhakika na ubora.

(a) Je, tokea lini Serikali ililitambua jambo hili.

(b) Ni lini tatizo hili litapatiwa ufumbuzi wake.

261. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari ni miongoni mwa sekta zinazokuwa kwa kasi duniani.

Je, Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha inaenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya habari duniani.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

50. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Tunafahamu kwamba nchi haiwezi kupata maendeleo ikiwa haikuwekeza katika viwanda. Viwanda ni moja ya eneo muhimu linalozalisha ajira na kuchochea maendeleo ya nchi.

(a) Je, ni ipi tathmini ya viwanda ambavyo vimekuwepo Zanzibar tokea Serikali ya Awamu ya Kwanza na upi mchango wao kwa maendeleo ya Zanzibar.

(b) Je, ni sababu gani zilizopelekea baadhi ya viwanda kufunga shughuli zao hapa Zanzibar na kuzihamishia Tanzania bara.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuviendeleleza viwanda vilivyopo Zanzibar.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

28. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Daraja la Chamanangwe Chake limekuwa ni moja ya eneo hatarishi katika barabara inayotoka Chake – Madenjani ambalo limekuwa moja ya chanzo cha watu wengi kupoteza uhai na wengine kubaki na ulemavu wa maisha. Madereva wengi wanasema moja ya tatizo kubwa ni mteremko mkali na mwembamba wa daraja lenyewe.

(a) Je, kwa kiwango gani Serikali inaitambua changamoto ya daraja hilo.

(b) Ni upi mpango wa Serikali wa haraka wa kupunguza ajali na vifo vinavyoweza kuepukika katika eneo hilo.

(c) Ni lini Serikali italijenga daraja hilo liwe la kisasa ili kuondoa tatizo lililopo hivi sasa.

73. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tumeona ukarabati wa barabara zetu baada ya kutumika kwa muda mrefu.

Ni wataalamu wepi wanaotumika kujenga barabara zetu.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

252. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Je Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha bahari yetu inatumika katika kupunguza changamoto ya ajira kwa vijana.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

167. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Jumla ya Watalii laki saba na elfu thelathini (730,000) walipokelewa mwezi wa Januari, 2025 hapa Zanzibar.

(a) Je, Wizara yako inafanya tathmini yoyote ya kujua ni nchi zipi zinazoongoza kwa watalii wake kufika hapa Zanzibar.

(b) Je, kuna tathmini yoyote iliyofanywa na inaeleza vipi juu ya kufunguka kwa masoko mapya ya utalii kufuatia ongezeko la watalii wanaofika nchini.

**Zanzibar,**
**11 Juni, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**